

**Kwa Rais wa Wanaverniana**  
**Nakala kwa Wenyeviti wote**  
**Isomwe kwa wanaverniana wote**

**MKUTANO MKUU wa V wa WANAVERNIANA**  
**2019**

Wapendwa wanakamati na Walei Wanaverniana wote,

hatimaye tunakaribia kufika kwenye tukio la Mkutano Mkoo wa tano wa Chama chetu, utakaofanyika mwishoni mwa mwaka 2019.

Mkutano wa Kamati kuu ya tarehe 05.10.2018 tayari umesaidia kutatua shida zote za kimazingira na kimipango, ambazo daima hazikosekani unapoandaa tukio kama hili.

*Katiba cha Chama chetu*, ibara 4.4, na *Mwongozo wa Mkutano Mkoo*, kipengele 1.1, ambavyo tunaweza kuviangalia hata kwenye mtandao “laicoverniani.net”, vinatukumbusha kuwa kazi ya Mkutano Mkoo ni

- **Kumteua Rais Mkoo na Wanakamati wanne; kati yao, wa kwanza atakuwa Makamu wa Rais;**
- **Kuthathmini maendeleo ya Chama;**
- **Kupanga mpango wa miaka 4 ijayo.**

Basi, nikiwa mwaminifu kwa Mwongozo, kipengele namba 3.2 na Katiba ibara namba 8, nikiwa nakibali cha Kamati Kuu,

**NATANGAZA RASMI**  
**MKUTANO MKUU WA V WA WANAVERNIANA**

UTAKAOANZA ALHAMISI 24 OKTOBA 2019, MCHANNA, HUKO ROMA, KATIKA NYUMBA YA MAFUNGO YA VIA DI VALCANNUTA 200, NA UTAKWISHA TAREHE 27 OKTOBA, JUMAPILI, BAADA YA CHAKULA CHA MCHANNA.

Mada kuu itakuwa:

**“Kukuza mbegu ya imani na matumaini katika nyakati zetu”**

Mada ya Mkutano Mkoo wa Masista (Julai 2018) inaendana na mada hiyo.

Kama mnavyojuu, kwenye mkutano mkoo watahudhuria “**Waakilishi wasiohitaji kuchaguliwa**” (Rais Mkoo, Wanakamati Wakuu na Rais wa Kanda zote), “**Waakilishi wanaochaguliwa**”, kutoka kila Kanda na “**Wasikilizaji**” (rejea Katiba 4.4 na Mwongozo 2.1 2.2).

Kila Kanda ya Wanaverniana itamteua mwakilishi **mmoja** (1).

**Kanda za Regioni Piemonte, Calabria ed Argentina** watawateua waakilishi **wawili** (2), kadiri ya Mwongozo, kama unavyonukuliwa hapo chini:

**2.1 Wanachaguliwa Walei wanaverniana waliopigwa kura katika kila Kanda.**

*Kila Kanda ina haki ya kuwa angalau mwakilishi mmoja, ambaye atahudhuria Mkutano Mkoo. Endapo Kanda fulani ina zaidi ya Wanaverniana 50, inawezekana apewe haki ya kumteua mwakilishi wa pili, jinsi atakavyoamua Rais Mkoo na Kamati yake. Hata hivyo, kila Kanda haitaweza kuchagua zaidi ya mwakilishi mmoja.*

*Uchaguzi unapaswa kufanyika angalau miezi mitatu kabla ya Mkutano Mkoo (...) Endapo aliyeteuliwa anakataa, kwa sababu zisizozuilkia, atachaguliwa yule anayemuata kadiri ya idadi za kura.*

*Katika uchaguzi, kiasi cha kura kwa ajili ya ushindi kinategemea idadi ya watu waliopo kwenye mkutano. Majina ya waliochaguliwa inabidi yafike mara moja kwa Rais Mkuu.*

**2.2 Wasikilizaji.** *Wasikilizaji wanaweza kuhudhuria mkutano na kazi za vikundi pia, kadiri Mkutano Mkuu utakavyoamuru. Lakini hawataweza kuwepo wakati wa kupiga kura. Wanaweza kuongea kwenye mkutano, ila hawawezi kupiga wala kupigwa kura.*

**Katika kipindi hiki cha maandalizi Wahusika wakuu ni Marais wa Kanda;** (wao wamepewa barua yao ya tofauti).

**Kwa sababu za mandalizi mengine (kwa mfano, kutuma mialiko kwa wateuliwa kutoka nchi za nje) Kamati Kuu inawasitisiza Marais wote kuteua MAPEMA IWEZEKANAVYO waakilishi, kabla ya tarehe 15 aprilii 2019.**

Ni muhimu sana kuwa **majibu ya maswali**, yakiandaliwa na Kundi zote za kiverniani ,zifike kwa Rais Mkuu au kwa Katibu Mkuu, aiu kwa sr. Maria Mori (yale ya kiswahili) kabla ya tarehe 15 machi 2019. Wahusika katika kazi hii ya kufikisha hayo, kwa njia ya posta au barua pepe, ni Marais wa Kanda.

Marais wa Kanda watatoa taarifa ya majina ya **wasikilizaji au wasindikizaji**, ili vyumba vyaa huko Valcannuta viandaliwe mapema.

“Mkutano Mkuu” utakuwa na kazi kubwa ya kuandaa mpango wa miaka 4 ijayo, kuendana na nyakati zetu. Maang’amu yetu yametufundisha kuwa Mikutano Mikuu yenyeye mafanikio zaidi ni ile ambayo imeandaliwa vizuri zaidi; kwa sababu hiyo, sote tuwajibike katika mandalizi hayo, kwanza Wenyeviti hadi Walei wote wa kila kikundi.

**Ili tuadhmishe mkutano mkuu wenyeye mafanikio, ni lazima tujiandae vema na mapema kiroho; sala inabidi itusindikize katika miezi hii ya maandalizi.**

Con l’auspicio che “il seme della speranza e della fiducia” guidino i nostri lavori e animino e rivivifichino la nostra Associazione nel futuro, a nome del Consiglio vi porgo i migliori saluti,

**Kwa niaba ya Wanakamati wote,**  
Mario V.Trombetta

Tumawaomba Kila Rais na Kila Mwenyekiti atoe taarifa ya kuwa amepata barua hii.